PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

PPAA
Toleo Na: 04 Januari - Machi 2025

# BULLETIN

UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## Tuitumie vyema Moduli ya kuwasilisha na kushughlikia rufaa

MPENDWA msomaji ni furaha yangu kukualika tena ujisomee toleo la nne la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA). Jarida hili hutumika kama njia mojawapo ya Mawasiliano ya Kimkakati ya PPAA katika kuhabarisha umma kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu.

Napenda kukujulisha katika kipindi hiki cha miezi mitatu (Januari – Machi, 2025) PPAA imetekeleza shughuli mbalimbali husussan, uzinduzi rasmi wa matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufaa na malalamiko kwa njia ya kielektroniki (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).

Pamoja na mambo mengine, PPAA imetoa mafunzo ya matumizi ya moduli ili kuwawezesha wazabuni kuwasilisha kielektroniki malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma. Pia PPAA imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kushughulikia rufaa zilizowasilishwa mbele yake katika kipindi tajwa.

Sanjari na mafunzo, pia jarida hili litakupa taarifa muhimu kupitia Habari na makala zinazohusiana na ununuzi wa umma ili kuongeza uelewa wa masuala ya ununuzi wa umma kwa kuwa sekta hii hutumia takribani asilimia 70 ya bajeti ya serikali.

Karibu tena usome jarida hili ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli mbalimbali ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Januari–Machi, 2025) na kuendeleza ushirikiano imara katika sekta ya ununuzi.

***#Kazi Iendelee.***

# PPAA yapewa changamoto kuokoa fedha za Serikali katika miradi

**RAIS Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete ameipa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) changamoto ya kuangalia jinsi ununuzi wa umma unavyoweza kuokoa fedha za umma na kuhakikisha kuwa serikali inapata thamani ya fedha katika miradi yake inayoitekeleza.**

Mheshimiwa Kikwete ametoa changamoto hiyo wakati alipotembelea banda la PPAA katika maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyoanza tarehe 25 Januari, 2025 katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

"Wakati nilipokuwa Rais kuna halmashauri moja ilijenga jengo lake kwa kutumia Shilingi milioni 15 kwa jitihada zao wenyewe, lakini wakaambiwa kwamba wasiendelee na utaratibu ule lazima zabuni itangazwe, baada ya zabuni kutangazwa wakanionesha nyumba iliyojengwa kwa milioni 45," amesema Dkt. Kikwete.

Hivyo kuna umuhimu wa wadau wa sekta ya ununuzi wa umma kuhakikisha sheria ya ununuzi wa umma inasaidia kupatikana kwa thamani halisi ya fedha katika miradi mbalimbali.

Afisa Mwandamizi wa PPAA, Bw. Stanley Jackson amemweleza Mhe. Dkt. Kikwete kuwa kwa kipindi cha takribani miaka minne, PPAA imeweza kushughulikia mashauri 162 yaliyotokana na michakato ya ununuzi wa umma ambapo katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 35 za thamani ya takribani Sh bilioni 583.6 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika.

"Hatua hiyo iliepusha utekelezaji usioridhisha wa miradi unaosababisha upotevu wa fedha za umma na

*Inaendelea Uk 2*




*Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete akipokelewa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Jaji Mstaafu Mhe. Sauda Mjasiri alipotembelea banda la mamlaka hiyo wakati wa uzinduzi wa maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyoanza tarehe 25 Januari, 2025 katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*

BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 04 Januari - Machi 2025

# PPAA yapewa changamoto kuokoa fedha

*Inatoka Uk 1*

kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi," amesema Bw. Jackson.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Jackson amesema PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imekamilisha utengenezaji wa moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufaa na malalamiko kwa njia ya kielektroniki (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).

Bw. Jackson ameongeza kuwa, kukamilika kwa moduli hiyo kutawawezesha wazabuni kuwasilisha kwa njia ya kielektroniki malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma kwa taasisi nunuzi na PPAA pasipo kulazimika kutembelea ofisi husika.

"Ili kuwawezesha wazabuni na watendaji wa taasisi nunuzi kutumia moduli hiyo, PPAA kwa kushirikiana na PPRA imeandaa mafunzo ya matumizi ya moduli ya kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki yatakayoambatana na tamko rasmi la kuanza kwa matumizi ya moduli hiyo.

Mafunzo haya yanawalenga wazabuni na watendaji wa taasisi nunuzi wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Musoma, Geita na Simiyu. Mafunzo yatafanyika kuanzia tarehe 4 - 6 Februari, 2025 jijini Mwanza katika Ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) uliopo Capripoint," aliongeza Bw. Jackson.

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yameongozwa na Kauli Mbiu: "Tanzania ya 2050: Nafasi ya Taasisi zinazosimamia Haki Madai katika kufikia Malengo Makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo."

PPAA ni taasisi inayojitegemea chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 112 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya mwaka 2023. PPAA imepewa kisheria jukumu la kupokea na kusikiliza malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma na kufungiwa kwa wazabuni (blacklisting of tenderers) kushiriki katika michakato ya ununuzi wa umma na PPRA.


BULLETIN
Toleo Na: 04 Januari - Machi 2025
Tuitumie vyema Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufaa
PPAA yapewa changamoto kuokoa fedha za Serikali katika miradi

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Florida Mapunda

Mhariri
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

Wajumbe
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga

Katibu
Nelson Kessy

Mawasiliano:
Katibu Mtendaji
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz

# PPAA mguu sawa kurasimisha matumizi ya moduli Kanda ya Ziwa

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewasihi wadau wa Ununuzi wa Umma Mikoa ya Kanda ya Ziwa kushiriki mafunzo ya matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufaa na malalamiko kwa njia ya kielektroniki katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) tarehe 4 – 6 Februari, 2025 Jijini Mwanza.**

Rai hiyo imetolewa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipozungumza na waandishi wa Habari katika maonesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea katika viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma na kuongeza kuwa mafunzo hayo yataambatana na tamko rasmi la kuanza kwa matumizi ya moduli hiyo.

Bw. Sando amesema kuwa, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imekamilisha moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufaa na malalamiko kwa njia ya kielektroniki (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa NeST.

"Mafunzo ya matumizi ya moduli kwa Kanda ya Ziwa yanawalenga wazabuni na watendaji wa taasisi nunuzi wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Musoma, Geita na Simiyu. Mafunzo yatafanyika kuanzia tarehe 4 - 6 Februari, 2025 Jijini Mwanza katika Ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) uliopo Capripoint," alisema Bw. Sando

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando ameongeza kuwa mafunzo kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia rufaa na malalamiko kwa njia ya kielektroniki katika Mfumo NeST yataendelea kwa kanda nyingine za kaskazini, kati, nyanda za juu kusini pamoja kusini.

Aidha, Bw. Sando alitoa wito kwa wadau wa kanda nyingine ambazo hazijapatiwa mafunzo kujiandaa kwani watafikiwa na kupatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya Moduli hivi karibuni.

Awali malalamiko na rufaa zilikuwa zinawasilishwa na mzabuni kwa kufika katika Ofisi za PPAA Jijini Dodoma. Aidha, kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 kuweka sharti la lazima la kufanya ununuzi wa umma kieletroniki, PPAA kwa kushirikiana na PPRA imejenga moduli itakayotumika kuwasilisha malalamiko na rufaa kieletroniki bila kuwa na ulazima wa kufika katika ofisi za PPAA.

Mei 28 - 29, 2024 Mafunzo ya matumizi ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki yaliandaliwa na PPAA kwa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga Morogoro na Pwani.

# Dkt. Mwigulu azindua Moduli ya Kupokea Rufaa Kielektroniki

**WAZIRI wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.) amezindua rasmi matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Kielektroniki (NeST).**

Dkt. Mwigulu amezindua rasmi matumizi ya moduli hiyo jijini Mwanza wakati wa mafunzo ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika mfumo wa NeST.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga amesema kuanza rasmi kwa matumizi ya moduli kuna faida kadhaa zikiwemo kuokoa muda, gharama, kupunguza mianya ya rushwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma.



"Moduli hii mpya inalenga kurahisisha zoezi zima la uwasilishaji wa malalamiko na rufaa kwa upande wa wazabuni na pia itawezesha taasisi nunuzi na PPAA kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia moduli hii, hivyo kupunguza muda na gharama zinazoambatana na zoezi zima la utoaji wa haki," amesema Dkt. Mwigulu.

Dkt. Mwigulu ametoa rai kwa wazabuni wote nchini pamoja na taasisi nunuzi kuwa tayari kujifunza na kutumia moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki ili kuokoa muda na fedha ambazo zingetumika katika uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi imara wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, PPAA imeshughulikia mashauri 162 yaliyotokana na michakato mbalimbali ya ununuzi wa umma.

"Katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 35 zenye thamani ya takriban Shilingi bilioni 583.6 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando ameongeza kitendo cha kuzuia tuzo kwa wazabuni hao kiliiepusha serikali kuingia katika mikataba ambayo ingepelekea kuwa na utekelezaji wa miradi usioridhisha hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi.

"PPAA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, imeweza kushiriki katika kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2025," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando ameongeza kuwa, ili kuendana na mabadiliko yaliyoletwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma, PPAA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, imeandaa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 ambazo zimetangazwa kwenye Gazeti la tarehe 31/01/2025 kupitia Gazeti la Serikali (GN No.65/2025).

Mafunzo hayo ya siku tatu yaliyoanza tarehe 04–06 Februari, 2025 yameandaliwa na PPAA.

Awali mafunzo ya matumizi rasmi ya moduli awamu ya pili kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa yametanguliwa na mafunzo ya awamu ya kwanza yaliyofanyika Mei, 2024 kwa mikoa ya Kanda ya Pwani iliyojumuisha Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.



*Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga akiwasilisha hotuba kwa wazabuni na taasisi nunuzi kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.) wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko kielektroniki kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa tarehe 04 Februari 2025, jijini Mwanza.*

# Wataalamu Ununuzi, Ugavi waaswa kuzingatia Maadili

**WATAALAMU wa sekta ya ununuzi wa umma wameaswa kuzingatia maadili ya taaluma yao katika usimamizi wa miradi ya umma ili kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha katika miradi yake.**

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda katika hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Mhe. Hassan Masala wakati wa kufunga mafunzo ya Moduli ya uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Kielektroniki (NeST) yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA).



*Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Mhe. Hassan Masala akifunga mafunzo ya moduli ya uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Kieletroniki (NeST) yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) jijini Mwanza.*

Mhe. Mtanda amesema kuzingatia maadili ya taaluma ya fani hiyo katika usimamizi wa miradi ya umma si tu kutaiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha bali kutaiheshimisha fani ya ununuzi na ugavi na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Kwa kuwa matumizi ya moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa kielektroniki huokoa muda, gharama na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika michakato ya zabuni za umma, nendeni mkaitumie elimu hii kuwaelimisha na wengine ili waweze kuielewa na kuitumia moduli, naamini ninyi mlioshiriki mafunzo ya awamu hii mtakuwa mabalozi wazuri wa moduli hii na PPAA kwa ujumla," amesema Mhe. Mtanda.

Naye Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema baada ya serikali kujenga mfumo wa NeST na kuweka sharti la lazima kufanya ununuzi wa umma katika mfumo huo, PPAA nayo ilishirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kujenga moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kielektroniki ili kuwawezesha wadau wa ununuzi wa umma kuwasilisha malalamiko na rufaa zao kielektroniki.

"Katika kipindi cha siku tatu washiriki wamejifunza masuala muhimu kuhusu mfumo wa ununuzi wa umma nchini Tanzania ikiwemo kuitazama kwa ufupi Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, kufanya mapitio ya mfumo wa NeST pamoja na namna ya uwasilishaji wa malalamiko na rufaa kwa kutumia moduli katika hatua mbalimbali," amesema Bw. Sando.



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na washiriki wa mafunzo.*



*Aliyekuwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Jaji Mstaafu Mhe. Sauda Mjasiri akizungumza na washiriki wa mafunzo*

Bw. Sando ameongeza kuwa washiriki wa mafunzo wamejifunza moduli ya uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa ambayo inajumuisha maeneo ya uwasilishaji wa malalamiko kwa Afisa Masuuli wa taasisi nunuzi iliyotangaza zabuni, uwasilishaji wa rufaa kwa PPAA.

Maeneo mengine ni jinsi mzabuni anavyoweza kujiunga katika rufaa iliyofunguliwa, taratibu za uwasilishaji wa maombi mbalimbali ikiwemo ombi la nyongeza ya muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda ulioainishwa katika sheria, ombi la kutengua uamuzi uliotolewa kwa kusikiliza shauri la upande mmoja na ombi la kukazia hukumu.

"PPAA imejipanga vyema kuendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya moduli kwa wadau wa ununuzi nchini kupitia kanda mbalimbali, hivyo wale ambao hawajafikiwa wajiandae kwani tutawafikia kupitia kanda zao zikiwemo kanda ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini, Kusini na Kati," ameongeza Bw. Sando.

Mafunzo hayo ya siku tatu yaliyojumuisha washiriki zaidi ya 580 yamefanyika mkoani Mwanza kuanzia tarehe 4 – 6 Februari, 2025 yakijumuisha mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Simiyu na Shinyanga.

Awamu ya kwanza ya mafunzo ya matumizi ya moduli iliyofanyika Mei 2024 kwa mikoa ya kanda ya Pwani iliyojumuisha Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.

BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 04 Januari - Machi 2025

# PPAA yatumia R4 za Rais Samia kuimarisha Haki, Uwazi, Uwajibikaji Ununuzi wa Umma

**NI miaka minne tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani chini ya uongozi imara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

Itakumbukwa kuwa Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia iliingia madarakani tarehe 21 Machi 2021 na wakati wote imekuwa ikisisitiza na kusimamia uwazi na uwajibikaji katika sekta ya ununuzi wa umma kuhakikisha rasilimali zinatumika kwa tija na kuwaletea wananchi maendeleo kwa wakati uliokusudiwa.

Tukiwa tunaadhimisha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, tunaangazia mafanikio ya moja kati ya taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi wa umma ambayo ni Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA).

PPAA ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya Umma Namba 3 ya Mwaka 2001 ambapo baada ya sheria hiyo kufutwa, Mamlaka ya Rufani ilihuishwa chini ya Sheria ya Ununuzi ya Umma Namba 21 ya Mwaka 2004 na kuhuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 7 ya Mwaka 2011 baada ya Sheria Namba 21 ya Mwaka 2004 nayo kufutwa.

Mwaka 2023 Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 7 ya Mwaka 2011 nayo ilifutwa na PPAA ilihuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya Mwaka 2023.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, jukumu kuu la PPAA ni kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya malalamiko au rufaa zitokanazo na maamuzi ya maafisa masuuli wa taasisi mbalimbali za umma katika michakato ya ununuzi wa umma.

Pia, ina jukumu la kupokea na kusikiliza malalamiko ya wazabuni ambao hawakuridhishwa na uamuzi wa kufungiwa (blacklist) na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi imara wa Rais Dkt. Samia imeendelea kudumisha, misingi ya utawala bora ikiwemo haki na usawa, pamoja na kuendelea kusimamia miradi ya kimkakati yenye tija kwa nchi na hivyo kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa umma.

Ikiwa takribani asilimia 70 ya bajeti ya serikali hutumika kwa ajili ya ununuzi wa umma, sheria, kanuni na miongozo ya ununuzi wa umma zinaiwezesha serikali kuendelea kuimarisha sekta ya ununuzi.



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,*
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,*

Katika kipindi cha uongozi wa Rais Dkt. Samia, PPAA imeendelea kutekeleza jukumu lake kuu la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma kwa haki, uwazi, uadilifu na kwa muda mfupi ili kuwezesha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha na kufikia malengo ya kutoa huduma bora kwa wananchi kwa wakati.

PPAA chini ya uongozi imara wa Rais Dkt Samia imefanikiwa kutekeleza majukumu yake katika maeneo ya falsafa ya R Nne (4R) kama ifuatavyo:

### i. Usuluhishi wa Migogoro (Reconciliation)

Katika kipindi cha miaka minne (4) ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, PPAA imeweza kushughulikia mashauri 171 yaliyotokana na michakato ya ununuzi wa umma. Aidha, katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 36 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika. Hatua hiyo iliepusha utekelezaji usioridhisha wa miradi unaosababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi.

Serikali ya Awamu ya Sita inaamini kuwa usuluhishi wa migogoro hauwezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia. Hivyo, kitendo cha PPAA kuzuia utoaji wa tuzo kwa wazabuni 36 waliokosa sifa kinaweka uzito katika usuluhishi wa migogoro ambayo ni moja kati ya falsafa za Rais Dkt. Samia.

PPAA imeendelea pia kudhibiti taasisi nunuzi kukiuka taratibu za kisheria hasa katika kufanya tathimini ya zabuni (tender evaluation); katika baadhi ya mashauri, PPAA ilifanikiwa kubaini ukiukwaji wa taratibu za kufanya tathimini uliofanywa na taasisi nunuzi ikiwemo kutokuzingatia vigezo vilivyowekwa katika kabrasha la zabuni au kuongeza vigezo vipya ambavyo havikuwepo awali.

### ii. Mageuzi (Reform)

Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na kuruhusu hatua za mageuzi kuchukuliwa pale ambapo ilibainika kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu katika mchakato wa ununuzi. Kupitia sheria mpya ya ununuzi wa umma mageuzi mbalimbali yalifanyika yakiwemo:

*Inaendelea Uk 6*

# PPAA yatumia R4 za Rais Samia kuimarisha Haki, Uwazi, Uwajibikaji Ununuzi wa Umma

*Inatoka Uk 5*

**a)** Kupunguza muda wa ushughulikiaji malalamiko au rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma. Mfano, muda wa siku saba (7) za kazi kwa ajili ya kusubiri malalamiko ya wazabuni (cool off period) kabla ya kutoa tuzo umepunguzwa na kuwa siku tano (5) za kazi. Muda huo hautajumuisha njia za ununuzi ambazo hazihitaji ushindani ambazo ni single source, minor value procurement na shopping; muda wa Afisa Masuuli kushughulikia malalamiko ya zabuni pia umepunguzwa kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi na pale ambapo Afisa Masuuli ataunda jopo la mapitio malalamiko basi atakuwa na siku saba (7) za kazi za kushughulikia na atatakiwa kuwajulisha washiriki wa zabuni kuwepo kwa jopo; na muda wa PPAA kushughulikia malalamiko au rufaa kutoka siku arobaini na tano (45) hadi siku arobaini (40).

**b)** Kuweka masharti ya lazima kwa taasisi nunuzi kufanya ununuzi kupitia mfumo wa kielektroniki. PPAA imefanikiwa kuanzisha moduli mpya ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kielektroniki (Complaint & Appeal Management). Moduli hiyo inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko na kutoa fursa kwa wazabuni wengi zaidi kuwasilisha malalamiko yao. Aidha, moduli hiyo ni rafiki na inaokoa muda wa kuwasilisha malalamiko. Moduli ya Complaint & Appeal Management imewekwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST), uliojengwa chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Ili kuwezesha matumizi ya moduli kwa ufasaha, PPAA iliweza kufanya mafunzo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa washiriki kutoka katika taasisi nunuzi na wazabuni takribani 913 wa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Pwani yaliyofanyika jijini Dar es Salaam Mei 2024 pamoja na Kanda ya Ziwa ikiwemo Mwanza, Shinyanga, Kagera, Musoma, Geita na Simiyu yaliyofanyika Februari, 2025 jijini Mwanza yakiwahusisha maafisa ununuzi, wakuu wa vitengo vya ununuzi, wakuu wa vitengo vya sheria, maafisa sheria, maafisa tehama, mawakili na wazabuni.




*Bw. James Sando.*
*Katibu Mtendaji – PPAA*

**c)** Matumizi ya (Tehama) Moduli ya Kielektroniki

Februari, 2025 serikali kupitia Wizara ya Fedha ilizindua rasmi matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika Mfumo wa NeST jijini Mwanza kwa wazabuni na taasisi nunuzi za mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Mwanza, Shinyanga, Kagera, Musoma, Geita na Simiyu.

Katika hotuba ya Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba iliyosomwa kwa niaba yake na Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Fredrick Mwakibinga, alisema kuanza rasmi kwa matumizi ya moduli kuna faida kadhaa zikiwemo kuokoa muda, gharama zilizokuwa zikiingiwa wakati wa uwasilishaji wa rufaa na majibu ya hoja za rufaa, kupunguza mianya ya rushwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma.

Faida nyingine ni kuwawezesha wahusika katika shauri kufuatilia na kufahamu hatua zote za uchakataji wa shauri linaloendelea.

**d)** Kutungwa kwa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma

Katika Kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Fedha, imeiwezesha PPAA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, kuandaa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2025 ambazo zilitangazwa kwenye gazeti la tarehe 31/01/2025 kupitia Gazeti la Serikali (GN No.65/2025).

### iii. Kujenga upya (rebuild)

Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha na kuboresha usimamizi wa sekta ya ununuzi wa umma nchini, hatua ambayo imeiwezesha PPAA kuwajengea uwezo wajumbe wa Mamlaka na watumishi wake na kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia vifaa muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya PPAA na kuiwezesha serikali kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa wakati.

### iv. Ustahimilivu (Resilience)

Licha ya athari za kiuchumi zilizoikumba na zinazoendelea kuikumba dunia na kutikisa uchumi kama Covid-19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja na kuadimika kwa fedha za kigeni (USD), bado Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuiwezesha PPAA kustahimili athari hizo na kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

# Wajumbe Kamati ya Bajeti Baraza la Wawakilishi Zanzibar ziarani PPAA



*Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Mb) akizungumza katika kikao kazi baina ya wajumbe wa baraza hilo na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kilichofanyika katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma.*

**WAJUMBE wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar wamefanya ziara ya kikazi ya siku moja katika Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) jijini Dodoma kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujifunza namna PPAA inavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma.**

Ujumbe huo umeongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Mb.), kadhalika, kamati hiyo iliambatana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Juma Makungu Juma (Mb.)

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ameeleza lengo la ziara hiyo ni kujifunza na kupata uzoefu wa PPAA katika sekta ya ununuzi pamoja na mnyororo wa ununuzi wa umma nchini.

Pamoja na mambo mengine, Mhe. Bi. Mwanaasha Khamis Juma amesema kamati hiyo itaendelea kushirikiana na PPAA na kuhakikisha kuwa zinasaidia serikali za pande zote mbili (Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, SMZ na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, SMT) kupata thamani halisi ya fedha katika miradi yake.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Mhe. Jaji Mstaafu Sauda Mjasiri alipongeza kamati hiyo kwa kuichagua PPAA kama moja ya taasisi ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa utekelezaji wa majukumu yake.

Naye Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando ameelezea historia ya PPAA, utekelezaji wa majukumu, changamoto na mafanikio ya mamlaka katika utumishi wa umma tangu kuanzishwa kwake.

Bw. Sando ameieleza kamati hiyo mkakati wa PPAA wa kuanzisha Moduli ya Kuwasilisha na Kushughulikia Malalamiko Kieletroniki (Appeal and Complaint Management Module) kwani moduli hiyo ni rafiki, inaokoa muda na gharama.

"Mhe. Mwenyekiti, awali wazabuni waliokuwa na malalamiko kuhusu zabuni walilazimika kufika katika Ofisi za Mamkala ya Rufani ya Zabuni za Umma, ila kwa sasa kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, kuweka sharti la lazima ununuzi wa umma kufanyika kielektroniki kupitia mfumo wa NeST, PPAA iliona ni vyema na yenyewe kuanzisha moduli ya kuwasilisha malalamiko kielektroniki ili kuwarahisishia wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kuwasilisha malalamiko yao kwa wakati," amesema Bw. Sando.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando ameieleza kamati hiyo kuwa PPAA imejipanga kuendesha mafunzo kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kielektroniki katika Mfumo wa NeST yataendeshwa kwa kanda ambazo ni Kanda ya Kaskazini, Kati, Nyanda za Juu Kusini na Kusini.

Kikao cha ziara ya kamati hiyo kilihudhuriwa na wajumbe wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, wajumbe wa Mamlaka ya Rufani, Menetimenti na Makatibu wa Kamati na baadhi ya watumishi wa PPAA.



*Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Wajumbe wa Mamlaka ya Rufani, Menejimenti ya PPAA wakiendelea na kikao kazi kilichofanyika katika Ofisi za PPAA Jijini Dodoma*



*Mwezeshaji wa mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Bi. Khadija Mzenzi akieleza jambo wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa PPAA. Mafunzo hayo yalifanyika katika ofisi za PPAA jijini Dodoma.*

# PPAA wapigwa msasa matumizi Mifumo ya TEHAMA

**ILI kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wamepatiwa mafunzo ya siku mbili kuhusu matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yaliyojikita katika saini ya kidijiti (digital signature) na mfumo wa usimamizi wa mkutano kieletroniki (e-Board).**

Akifungua mafunzo hayo katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amewasihi watumishi wa Mamlaka ya Rufani kutumia mafunzo hayo kama chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa kila siku.

"Matumizi ya Tehama katika ofisi yanasaidia kupunguza gharama na kuongeza ufanisi katika utendaji, lakini pia huwafanya watumishi kuwa salama zaidi katika utendaji kazi wao wa kila siku," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando ameongeza kuwa msisitizo wa matumizi ya Tehama ni muhimu kwani ndipo serikali ilipo hivyo ni vyema kama serikali ipo kwenye mifumo ya Tehama na PPAA kukaa serikali ilipo.

"Serikali imejipambanua kutumia Tehama katika utendaji wake ili kuwafikishia wananchi huduma bora kwa wakati. Hivyo, Tehama ni msingi wa utendaji kazi wa Serikali," amesema Bw. Sando

Kwa upande wake mwezeshaji wa mafunzo hayo wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Bi. Khadija Mzenzi, amewaasa watumishi kujitahidi wanapokuwa kazini kufanya kazi kwa kuzingatia Tehama.

"Tumekutana hapa kwa lengo la kuisaidia serikali, hivyo tupende kujifunza vitu vipya hususan katika Tehama ili kuwa wabobevu wa matumizi sahihi ya kidijiti kazini kuongeza ufanisi," amesema Bi. Mzenzi.

Naye Bw. Anthony Nchimbi mwezeshaji kutoka eGA ameongeza kuwa matumizi ya saini ya kidijiti (digital signature) huongeza uwajibikaji kazini kwani kwa kutumia teknolojia hiyo si rahisi mtumishi kufoji (forgery) saini ya kiongozi au mkuu wa taasisi hivyo husaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji wa moja kwa moja kwa mtumishi.

Mada zilizowasilishwa wakati wa mafunzo hayo ni pamoja na matumizi ya saini ya kidijili na kuandaa mkutano kwa njia ya kielektroniki.

# PPAA yashiriki Maadhimisho Siku ya Wanawake Duniani jijini Arusha

**WAKATI Tanzania imeungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake 2025, wanawake kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wameungana na wanzao kutoka ofisi mbalimbali za umma na binafsi kuadhimisha siku hiyo kitaifa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.**

Maadhimisho hayo hufanyika kila tarehe 08 Machi, yameandaliwa kwa lengo la kutambua mchango wa wanawake na kuhimiza usawa wa kijinsia katika jamii.

Maadhimisho hayo kitaifa yamefanyika jijini Arusha, yakiwa na kaulimbiu isemayo: "Wanawake na Wasichana Tuimarishe Haki, Usawa na Uwekezaji."

Aidha, kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu 2025 imeakisi lengo la kusherehekea mafanikio ya wanawake, kujadili changamoto wanazokabili pamoja na kutafuta njia za kuimarisha haki na usawa kwa maendeleo endelevu.

Mgeni Rasmi katika kilele cha maadhimisho hayo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema serikali imepiga hatua kubwa katika kufanikisha malengo ya kuhakikisha kesho bora na njema zaidi kwa vijana wa Kitanzania, wa kike na wa kiume.


Dkt. Rais Samia amesema kuwa Tanzania ina mengi ya kujivunia katika kuboresha mazingira yanayohakikisha ndoto ya usawa wa kijinsia inafikiwa nchini. "Tunapoadhimisha miaka 30 tangu Tamko la Umoja wa Mataifa la Mkutano wa Beijing, miaka 10 ya Malengo Endelevu ya Dunia na miaka mitano ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa, ni fursa ya kutathmini mafanikio makubwa yaliyofikiwa na kutambua hatua zaidi zinazohitajika ili kuhakikisha kila msichana na mwanamke hapa nchini anapata nafasi ya kufikia ndoto zake," alisema Rais Dkt. Samia.

Rais Samia amesisitiza kuwa hatua mbalimbali za kisera na kisheria zimechukuliwa na zinaendelea kuchukuliwa ili kupambana na mila kandamizi na ubaguzi dhidi ya wanawake na watoto wa kike.

"Watanzania, wake kwa waume, wameunga mkono maamuzi na hatua mbalimbali za kumwezesha mwanamke, hali ambayo imewezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa katika usawa wa kijinsia," aliongeza.

Akifafanua maendeleo yaliyopatikana, Rais Dkt. Samia alitaja hatua kubwa zilizochukuliwa katika sekta mbalimbali za maendeleo nchini, sambamba na Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

Alisema kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kupunguza umaskini, kukomesha njaa, kuboresha afya na ustawi, elimu bora, usawa wa kijinsia, maji safi na usafi, nishati mbadala, kazi zenye staha, ukuaji wa viwanda, ubunifu na miundombinu, pamoja na kuimarisha amani, haki na taasisi madhubuti.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwasalimia wanawake walioshiriki Siku ya Wanawake Duniani 2025, Kitaifa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Machi 08.*



*Wanawake wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) walioshiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 08, 2025 katika picha kabla ya kuanza maandamano ya kuelekea katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha*




*Baadhi ya Wanawake kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wakiwa na bango lao tayari kuanza maandamano ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 08 Machi, 2025 jijini Arusha.*

# Tume ya Taifa ya Umwagiliaji yashinda rufaa zabuni ukarabati miradi umwagiliaji

**TUME ya Taifa ya Umwagiliaji imeshinda rufaa iliyokatwa dhidi yake na kampuni ya Jisham Construction Co. Ltd kuhusu zabuni ya ukarabati wa miradi ya umwagiliaji ya Matarajira, Mtazamo, na Bahi katika Wilaya ya Bahi, Dodoma.**

Rufaa hiyo imesikilizwa na kutolewa uamuzi na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) Januari 2025 chini ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Mhe. Jaji Mstaafu Sauda Mjasiri.

Rufaa hiyo iliwasilishwa na kampuni ya Jisham Construction Co. Ltd baada ya kutoridhishwa na sababu za kuondolewa kwake kwenye mchakato wa zabuni kwa kushindwa kutimiza vigezo vya uzoefu na mahitaji ya vifaa kama ilivyoainishwa kwenye kabrasha la nyaraka ya zabuni.

Mrufani alieleza kuwa kuondolewa kwake kwenye mchakato wa zabuni kwa kushindwa kuambatanisha ushahidi wa umiliki wa vifaa vilivyotajwa kulisababishwa na mfumo wa NeST.

Alieleza hakukuwa na sehemu katika mfumo huo iliyoruhusu waombaji wa zabuni kuambatanisha ushahidi wa umiliki wa vifaa endapo mrufani anamiliki vifaa hivyo.

Aidha, alibainisha kuwa iwapo angeeleza amekodisha vifaa hivyo, mfumo wa NeST ungefungua sehemu ya kuambatisha mkataba wa ukodishaji wa vifaa. Kwa mantiki hiyo, mrufani alidai kuwa kushindwa kwake kuambatisha ushahidi wa umiliki wa vifaa kulitokana na kasoro ya mfumo wa NeST na hakupaswa kuadhibiwa kwa makosa ya mfumo.



Kuhusu kutokidhi hitaji la uzoefu, mrufani alieleza kuwa nyaraka za zabuni zilihitaji wazabuni kuonesha uzoefu wao katika kazi za ujenzi wa miundombinu ya kazi za ujenzi au umwagiliaji.

Katika kuthibitisha alikidhi hitaji hilo, aliwasilisha cheti cha kukamilika kwa mradi wa upanuzi wa bomba la maji la Ziwa Victoria hadi Tabora, Nzega, na Igunga. Pia, aliwasilisha cheti cha kukamilika kwa mradi wa upanuzi wa huduma ya maji ya Ziwa Victoria kwa vijiji vya Ndekeli, Mangashini, Tumbi, na Chabutwa.

Mlalamikaji alidai nyaraka za zabuni zilihitaji wazabuni kuonesha uzoefu wao katika miradi ya kazi za ujenzi au umwagiliaji. Aliongeza kuwa, kwa mujibu wa maneno yaliyotumika katika nyaraka za zabuni, ni wazi wazabuni walihitaji kuonesha uzoefu wao katika mojawapo ya maeneo hayo mawili.

Kwa kuwa amewahi kutekeleza miradi mbalimbali ya maji, alieleza kuwa uzoefu wake katika miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji unapaswa kukubalika, kwani miradi ya maji pia ni sehemu ya kazi za ujenzi kwani alikidhi hitaji la uzoefu kama ilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni na hakupaswa kuondolewa katika mchakato wa zabuni.

Kwa upande wake, Mrufaniwa alieleza kuwa wakati wa tathmini, ilibainika kuwa zabuni ya mrufani haikukidhi kigezo cha uzoefu. Pia, hakuwasilisha nyaraka zinazoonesha umiliki wa vifaa vilivyotajwa kama ilivyohitajika kwenye nyaraka za zabuni. Kutokana na sababu hizo, zabuni yake iliengulіwa kwa kutokidhi vigezo.

Katika kufafanua zaidi sababu za kuondolewa kwa zabuni ya mrufani, Tume ilieleza kuwa nyaraka za zabuni zilihitaji wazabuni waoneshe umiliki wa vifaa muhimu vilivyotajwa au uwezo wa kuvipata. Hata hivyo, mrufani hakuwasilisha nyaraka za kuthibitisha umiliki wa vifaa hivyo kama ilivyotakiwa, hivyo kushindwa kutimiza matakwa ya zabuni. Mrufaniwa alieleza katika rufaa hiyo, mrufani alishindwa kuambatanisha ushahidi wa umiliki wa vifaa vilivyotajwa na kudai mfumo wa NeST haukuwa na sehemu ya kuambatisha nyaraka za umiliki wa vifaa hivyo.

Aidha, mrufaniwa alifafanua kuwa wazabuni wengine wanaomiliki vifaa vilivyohitajika waliweza kuambatisha nyaraka zao za umiliki katika sehemu husika. Hivyo si kweli kwamba mfumo wa NeST haukuwa na sehemu ya kuambatisha nyaraka za umiliki wa vifaa.

Kadhalika, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliongeza kuwa, Sheria ya Ununuzi wa Umma inahitaji tathmini ya zabuni kufanywa kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa katika nyaraka za zabuni. Wakati wa tathmini ya zabuni, Tume ilizingatia vigezo vyote vilivyowekwa katika nyaraka za zabuni na kubainika kuwa zabuni ya mlalamikaji haikuwa na nyaraka za umiliki wa vifaa vilivyotajwa. Hivyo, kuondolewa kwake kwenye mchakato wa zabuni ilikuwa sahihi na kwa mujibu wa sheria.

Katika kufafanua kushindwa kwa mrufani kutimiza hitaji la uzoefu, mrufaniwa alieleza kuwa nyaraka ya zabuni zilihitaji wazabuni kuzingatia masharti yaliyotolewa katika nyaraka ya zabuni. Nyaraka ilieleza kuwa katika suala la uzoefu, wazabuni walihitaji kuonesha uzoefu wao katika kutekeleza mikataba yenye asili inayofanana kwa kuzingatia ukubwa, ugumu wa kazi, mbinu za utekelezaji, na mahitaji mengine kama yalivyoainishwa.

Aidha, wakati wa mchakato wa tathmini, ilionekana kuwa zabuni ya mrufani haikukidhi hitaji la uzoefu kama ilivyotakiwa katika nyaraka ya zabuni. Nyaraka ya zabuni ilihitaji mrufani kuwasilisha ushahidi wa kuwa na uzoefu wa kutekeleza miradi miwili ya umwagiliaji, kila mmoja ukiwa na thamani ya Sh bilioni mbili za Kitanzania, iliyotekelezwa kati ya mwaka 2021 hadi 2024. Badala yake, mrufani aliwasilisha uzoefu katika miradi ya maji, ambayo asili yake na mbinu za utekelezaji wake hazifanani na miradi ya umwagiliaji kama ilivyohitajika kwenye zabuni husika.

Katika kuamua rufaa, PPAA ilipitia kumbukumbu za rufaa na kubaini zabuni ya mrufani iliengulіwa kwa kushindwa kutimiza hitaji maalumu la uzoefu na kwa kutowasilisha nyaraka za umiliki wa vifaa vilivyoorodheshwa.

Kuhusu uthibitisho wa umiliki wa vifaa vilivyoorodheshwa, PPAA iligundua zabuni ya mrufani iliengulіwa kwa kushindwa kuonesha umiliki au uwezo wa kupata vifaa muhimu kama ilivyobainishwa katika nyaraka za zabuni.

PPAA ilifuatilia pia zabuni ya mrufani iliyowasilishwa kupitia NeST na kubaini mrufani alikuwa ameorodhesha vifaa vyote kama ilivyobainishwa kwenye nyaraka za zabuni.

Aidha, alieleza baadhi ya vifaa alikuwa anavimiliki binafsi na vingine vilikuwa vya kukodiwa. Kwa vifaa vya kukodi, mrufani aliambatanisha mkataba wa kukodi, ila vifaa vilivyodaiwa kuwa na umiliki binafsi, hakukuwa na nyaraka zozote zilizowasilishwa kuthibitisha umiliki wake.

Kuhusu ukosefu wa uzoefu, PPAA ilipitia nyaraka ya zabuni, hususan vigezo vya tathimini ya kiufundi vinavyotoa mwongozo kuhusu uzoefu unaohitajika. Ilibainika kuwa wazabuni walihitajika kuthibitisha uzoefu kwa kuonesha idadi ya chini ya mikataba yenye ulinganifu kwa kuzingatia ukubwa wa kazi, ugumu wake, na mbinu/ teknolojia iliyotumika katika utekelezaji wa mkataba.

Uzoefu pia ulitakiwa kuthibitishwa kwa kuwa na angalau mikataba miwili, kila moja ikiwa na thamani maalumu ya TZS bilioni mbili iliyotekelezwa kati ya tarehe 1 Januari 2021 hadi 30 Septemba 2024.

Ili kubaini iwapo mrufani alikidhi hitaji la uzoefu maalumu, PPAA ilipitia upya zabuni ya mrufani katika mfumo wa NeST na kubaini kuwa mrufani alikuwa ameambatanisha vyeti viwili vya kukamilika kwa miradi.

Aidha, baada ya kupitia vyeti vya miradi hiyo, PPAA ilibaini kuwa hakuna hata moja ya miradi hiyo uliokuwa unahusiana na miradi ya umwagiliaji. Hivyo, PPAA iliridhishwa na sababu za zabuni ya mrufani kuondolewa kwa kutokidhi kigezo cha uzoefu.

PPAA ilibaini pia kuwa zabuni ya mrufani iliengulіwa kwa kushindwa kutimiza kigezo cha uzoefu wa chini kabisa kama kilivyobainishwa kwenye nyaraka za zabuni.

Kwa msingi huo, PPAA imetupilia mbali rufaa hiyo kwa kushindwa kutimiza mahitaji husika na kuagiza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma.

# PPAA yaichapa PSPTB magoli matano bila huruma



*Wachezaji wa timu ya mpira wa miguu wa PPAA kabla ya kuanza mchezo wao dhidi ya PSPTB. Katika mchezo huo PPAA iliibuka mshindi kwa kufunga penalti zote tano (5) huku PSPTB ikiambulia penalti nne (4).*

**TIMU ya Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeibuka mshindi wa mchezo wa mpira wa miguu kupitia mikwaju ya penalti 5-4 dhidi ya timu ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) baada ya kutoa sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za mchezo.**

Mchezo huo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Serikali ya kudhibiti Ukimwi na magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) ambapo PPAA na PSPTB wamefanya mazoezi mbalimbali.

Michezo hiyo imefanyika tarehe 01 Machi, 2025 katika viwanja vya Kilimani Park, jijini Dodoma.

Michezo mingine iliyochezwa mbali na soka ni kukimbiza kuku, kukimbia kwa magunia na kuvuta kamba ambapo baada ya michezo hiyo washindi walikabidhiwa zawadi mbalimbali.

Kwa upande wa mpira wa miguu PPAA imeibuka mshindi wa kwanza baada ya kuchuana vikali na PSPTB.

Ushindi wa PPAA umepatikana kwa mikwaju ya penalti baada ya kutoka sare goli 1-1 katika dakika 90. Katika mtanange huo, PPAA ilianza kuongoza kwa goli lililofungwa dakika ya 18 ya kipindi cha kwanza na mchezaji machachari Dionis Nyaudo.

PPAA ilienda mapumziko ya kipindi cha kwanza ikiwa na goli moja kibindoni. Kipindi cha pili kilianza huku PSPTB wakiwa wana usongo wa kurudisha goli ambapo katika dakika ya 50 ya mchezo walipata goli kwa njia ya penati iliyopigwa baada ya beki wa PPAA kucheza madhambi kwa mchezaji wa PSPTB.

Hadi dakika 90 za mchezo zinaisha timu zote zilikuwa na goli moja na hivyo kupelekea mtanange huo kuamuliwa kwa penalti.

Katika penalti hizo, PPAA ilifanikiwa kufunga penalti zote tano (5) huku PSPTB ikiambulia penalti nne (4) kati ya tano (5). Hivyo kuifanya PPAA kuibuka mshindi wa mchezo huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB, Bw. Godfred Mbanyi amesema lengo la michezo au bonanza hilo ni kudumisha umoja na ushirikiano kwa watumishi wa taasisi hizo pamoja na kuimarisha afya za watumishi na kukabiliana na magionjwa yasiyoambukiza.

“Sisi PSPTB kwa kushirikiana na wenzetu wa PPAA tumeandaa bonanza hili la michezo ili kutuwezesha kutekeleza Sera ya Serikali ya kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza, kuimarisha afya zetu pamoja na kudumisha ushirikiano na umoja katika kuzijenga taasisi zetu,” amesema Bw. Mbanyi.

Kwa upande wake Mkuu wa Sehemu ya Utawala na Rasilimaliwatu kutoka PPAA, Bw. Mohamed Makame amewapongeza watumishi wa PPAA kwa kujitokeza na kushiriki kwa wingi bonanza hilo lililoandaliwa na PSPTB.

“PPAA tumekuwa tukitekeleza sera ya Serikali ya kufanya mazoezi kwa siku mbili kila wiki ambapo siku hizo ni Jumanne na Alhamisi.

Kutokana na mazoezi hayo yametuwezesha kuiwakilisha vyema taasisi yetu katika michezo mbalimbali husussan mbio za gunia ambapo PPAA tuliibuka washindi wa kwanza kupitia mwanariadha mahiri Bi. Rachel Sironga,” amesema Bw. Makame.

# HABARIPICHA

*Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete akieleza jambo kuhusu michakato ya zabuni za umma alipotembelea banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wakati wa uzinduzi wa maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*







*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na watumishi wa mamlaka hiyo alipowatembelea katika banda kwenye Maonesho ya Wiki ya Sheria katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*

*Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda akizungumza na viongozi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) walipomtembelea ofisini kwake kujitambulisha na kumwalika kwenye uzinduzi wa matumizi ya Moduli kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kielektroniki yaliyofanyika Februari 2025 jijini Mwanza. Ujumbe wa PPAA uliongozwa na Katibu Mtendaji Bw. James Sando. Wengine pichani ni Meneja wa Huduma za Kisheria PPAA, Bi. Florida Mapunda na Meneja wa Huduma za Fedha na Utawala PPAA, Bw. Paschal Kajuna.*






*Viongozi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), wakiongozwa na Katibu Mtendaji Bw. James Sando (katikati waliokaa) katika picha na watumishi wa mamlaka baada ya uzinduzi rasmi wa matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Kieletroniki (NeST) jijini Mwanza.*